



Unapojibu tafadhali taja;

Kumb: Na. SHY/MC/S. 20/47 VOL II/ 14

Tarehe: 22/03/2023.

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga anapenda kuwatangazia watazania wote kuwa amepokea Kibali cha Ajira mbadala chenye Kumb. Na. FA.170/376/01"B"/ 118 cha tarehe 06 Februari, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kujaza nafasi ya kazi ya **Dereva Daraja la II**. Hivyo watazania wote wenye sifa mnakaribishwa kutuma maombi ya kujaza nafasi hiyo kama ifuatavyo;-

DEREVA II NAFASI MOJA (1)

(i) Sifa za kitaaluma kwa mwombaji

- Awe na cheti cha kuhitimu na kufaulu Kidato cha Nne (IV), aliyepata mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- Awe na leseni daraja la "E au "C ya uendeshaji, mwenye uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- Mwenye cheti cha majaribio ya uendeshaji magari atapewa kipaumbele/kufikiriwa kwanza.

ii) Majukumu ya kufanya

- (a) Kuendesha magari ya Serikali kwa kuzingatia Kanuni za Usalama Barabarani
- (b) Kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ili kubaini ubovu unaohitaji matengenezo
- (c) Kuhakikisha kuwa gari pamoja na vifaa vyake (Jeki, Spana, Tairi la akiba n.k.) viko katika hali nzuri wakati wote
- (d) Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari.

- (e) Kuhakikisha kuwa gari limefungwa milango na vioo na liko salama wakati wote.
- (f) Kuhakikisha kwamba gari liko katika hali ya usafi ndani na nje wakati wote.
- (g) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari (Log Book).
- (h) Kuhakikisha kuwa gari limeegeshwa kwa wakati katika sehemu salama na sehemu zilizoidinishwa (Secure and Authorized Place) kwa mujibu wa Sheria na Kanuni.
- (I) Kutoa taarifa kuhusu ajali ya gari kwa Mkuu wake kwa wakati na Polisi wa kikosi cha Usalama Barabani cha Jeshi la Polisi.

(iii) **Masharti ya Ajira.**

Ajira ya Kudumu

(iv) **Mshahara.**

Ngazi ya mshahara wa kuanzia ni **TGS B.**

v) **Masharti ya jumla kwa waombaji.**

1. Awe raia wa Tanzania.
2. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 na asizidi miaka 45.
3. Mwombaji lazima aambatanishe wasifu wake binafsi (CV) akionesha mawasiliano yake ya uhakika, anwani, barua pepe na namba za simu.
4. Mwombaji anatakiwa kuwa na namba ya utambulisho wa uraia (National identification number) kutoka Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA).
5. Mwombaji aombe kwa kuzingatia masharti ya **TANGAZO LA KAZI.**
6. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Taaluma (Certificates), nakala ya cheti cha Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) kwa wale waliofika kiwango hicho cha Elimu, vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
7. Transcripts, Testimonials, Provisional Results, Statement of Results na Hati za matokeo ya Kidato cha IV au VI havitakubaliwa.
8. Mwombaji mwenye cheti cha Kidato cha Nne/Sita na Cheti cha Taaluma ambacho kimepatikana nje ya nchi; ahakikishe kuwa vyeti hivyo vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (**NECTA**) na Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (**NACTE**).


9. Nakala zote za vyeti vya taaluma na cheti cha kuzaliwa zithibitishwe na wakili aliyesajiliwa na kuthibitishwa.
10. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza.
11. Watakoachaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili.
12. Maombi yaambatane na picha mbili (passport size) za hivi karibuni. Picha iandikwe jina la mwombaji kwa nyuma.
13. Barua zote zitumwe kupitia Posta. Barua zitakazoletwa kwa mkono hazitapokelewa.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 05.04.2023 saa tisa na nusu (09:30) Alasiri.

Maombi yote yatumwe kwa:

**MKURUGENZI WA MANISPAA,
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA,
S.L.P. 28,
SHINYANGA.**

Tangazo hili limetolewa na;


John R. Tesha

KAIMU MKURUGENZI WA MANISPAA

**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
SHINYANGA**